

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**23 Mei 2009**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Juma Hassan Chibaya  
Mussa Alex  
Juma Ali Salehe Jongo  
Selion Elieskia  
Beda John Mkusu  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Shamte J Kigoma  
Dominata Rwechungura  
Mejah Mbuya  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Sosthenes C Amlima  
Husein Hamza Hamisi  
Juma Imori Rugole

**Mradi wa Wamba**

Elaine alileta vipeperushi 200 na wanachama walichukua ili kusambaza.

Mama Khadija atafanya chakula na chai kwa ajili ya mafunzo.

Tulitengeneza badjeti – Tsh 420,000 kwa reflekta jaketi, Tsh 480,000 kwa helmeti, Tsh 180,000 kwa posho, Tsh 158,400 kwa chai na chakula, Tsh 87,000 kwa photocopying.

Mejah na Juma watachukua Tsh 800,000 kutoka benki na kujumlisha na Tsh 100,000 ya hela za UWABA ambayo Mejah anayo. Filbert na Hamadi wataenda kununua jaketi na helmet.

**Re-cycle**

Mejah alileta mkataba ya ofisi TRA lakini sasa wanasema wanahitaji documents zingine ambazo hawajatuambia mwanzoni. Wanahitaji passport photos ambazo zimegongwa mihuri na serikali ya mtaa za Elaine na Mejah na vyeti vya TIN binafsi yao. Pia wanahitaji nakala ya katiba.

Serikali ya mtaa walishahihisha barua kwenda kwa mkuu wa wilaya. Elaine atarekebisha na Juma atafuatalia tena mihuri.

**Kongamano / JICA**

Juma alikuwa na umwa wiki hii. Atafuatalia wiki ijayo.

**Masuala ya barabara**

Mejah ataandika barua kuhusu marekebisho ya barabara Afrikana.

Kampuni ya kichina wanaofanya kazi za DAWASCO wameziba kabisa sehemu za service roads za Morogoro na kulazimisha wapanda baisikeli kwenda kwenye barabara kubwa.

### **Ushirika wa Fasta Cycle courier**

Bwana Bukuku alisema tukutane naye tarehe 5 mwezi wa sita.

### **Mkutano ya usalama barabarani**

Mejah alifuatalia na Adam Msinga lakini yupo Mbeya.

Wanaotayarisha mkutano wa usalama barabarani Dar es Salaam bado hawajajibu email kutujulisha wanachama wengapi wanaweza kuhudhuria.

### **Mkutano wa Tanga**

Mkutano wa Tanga itakuwa alhamisi. Wanachama wawili wa UWABA watapewa nafasi wakigawana per diem ya mtu mmoja. Wanachama walichagua Mejah na Dominata kuhudhuria. Uli Malisius ambaye alitualika UWABA aliomba kuona video ya cycle friendly cities kabla ya mkutano. Mejah na Dominata wataenda ofisini kwake jumatatu.

### **Ruzuku ya Foundation for Civil Society**

Juma alikuwa na umwa wiki jana – atapeleka maombi ya ruzuku wiki hii.

### **Video**

Mejah alipeleka kwa TBC, ITV lakini traffic police bado. Sosthenes alipeleka kwa Channel 10 na TANROADS mkoani – bado hajapeleka kwa Star TV wala DART. Filbert alipeleka kwa serikali ya jiji na wizara ya miundombinu. Juma bado hajapeleka kwa TANROADS makau makuu.

### **Wimbo**

Mejah ameanza kutayarisha CD cover. Elaine alileta CDs 10 za blank ofisini.

### **Cycle Generation**

Ragna wa Cycle Generation alitutumia petition kuhusu mabadalisho ya majria. Wanachama walisaini na Elaine atamtumia. Wamemaliza safari ya baisikeli kutoka Ethiopia mpaka Afrika Kusini.

### **Mambo ya hela na guta**

Filbert alileta Tsh 7,000 ya hela ya guta. Tsh 4,000 ilirudishwa kwa Elaine kwa gharama ya kufanya photocopy ya vipeperushi. Filbert ana Tsh 3,000 ya hela ya UWABA na Mejah ana Tsh 160,000. Guta imerekebishwa.